



**TUME YA
KUDHIBITI
UKIMWI
TANZANIA**



HABARIKA NA TACAIDS

**DAWA ZA KUFUBAZA VVU
ZINAPATIKANA KWA 100%**

Toleo Na. 002

Zarida Mtandao



DAWA ZA KUFUBAZA MAKALI ZINAPATIKANA KWA 100%

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu -Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, Mheshimiwa William Lukuvi, amewahakikishia Watanzania kuwa dawa za kufubaza makali ya Virusi Vya UKIMWI (ARVs) zinapatikana kwa asilimia 100 nchini, na zinatolewa bila VVU (WAVIU).

Amesema hayo Disemba 01, 2025 jijini Dar es Salaam wakati akitoa Tamko la Serikali katika maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani yenye kaulimbiu "Imarisha Mwitikio, Tokomeza UKIMWI."

Waziri Lukuvi amesema upatikanaji wa dawa hizo umeendelea kuimarika, huku idadi ya WAVIU wanaotumia dawa za ARV ikiongezeka kutoka asilimia 98 mwaka 2024 hadi asilimia 98.5 mwaka 2025, hatua inayochochea kupungua kwa athari za Maambukizi ya za wananchi.

Aidha, Waziri Lukuvi amebainisha kuwa Serikali imeongeza idadi ya vituo vinavyotoa huduma za tiba na matunzo kwa WAVIU ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za VVU na UKIMWI nchini. Vituo hivyo vimeongezeka kutoka vituo 7,805 mwaka 2024 hadi vituo 8,203 mwaka 2025.

Vile vile, huduma za ufuatiliaji wa matibabu kwa WAVIU zinaendelea kuimarishwa, huku Serikali ikiboresha upatikanaji wa huduma za maabara kwa kuongeza mashine za kupima wingi wa VVU mwilini. Kwa sasa, zipo mashine kubwa 50 kutoka 43 mwaka 2024, na mashine ndogo 127, hivyo kufanya kuwa na jumla ya mashine 177 zinazoendelea kutoa huduma kote nchini.

Katika tamko lake, Waziri Lukuvi amesisitiza kuwa Siku ya UKIMWI Duniani ni muhimu kwa kutathmini hali na mwelekeo wa kudhibiti VVU na UKIMWI nchini, kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya maambukizi mapya, kuwakumbuka waliopoteza maisha kutokana na ugonjwa wa UKIMWI na kuwaenzi watu wanaoishi na VVU pamoja na yatima wanaotokana na athari za UKIMWI.



TACAIDS YATOA MAFUNZO YA VVU NA UKIMWI KWA VIJANA WILAYA YA CHAMWINO

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania-TACAIDS kwa kushirikiana na Hal-mashauri ya Wilaya ya Chamwino pamoja na wadau chini ya ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa (UNFPA) imetoa mafunzo kwa vijana wa kata ya Dabalo wilayani Chamwino kuhusu ku-

sahihi ya Kondom, kupinga Unyan-yapaa na Ubaguzi kwa Watu Wanaoi-shi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) pamoja na kuinga maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na elimu kuhusu Mwitikio wa UKIMWI nchini.

Mafunzo hayo yamefanyika Disemba 03, 2025 kwa lengo la kuwaongezea vijana uelewa katika masuala muhimu ya VVU na UKIMWI ikiwa ni pamoja na kuhamasisha vijana kuzifikia huduma za UKIMWI kama vile upimaji, huduma za Kinga, Matibabu na Matunzo ili kufi-kia malengo ya kutokomeza UKIMWI kama tishio la afya ya jamii ifikapo mwaka 2030.





KILELE CHA MWENGE WA UHURU KUSISITIZA MAPAMBANO DHIDI YA VIRUSI VYA UKIMWI

Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2025 zimefikia tamati kwa kutoa msisitizo juu ya utoaji wa elimu na mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI nchini

Msisitizo huo umetolewa Oktoba 14, 2025 na kiongozi wa mbio za mwenge kitaifa Ismail Ali Ussi wakati akisoma risala ya kutamatisha mbio na kukabidhi rasmi Mwenge wa Uhuru kwa Mhe Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Philip Mpango, viwanja Sokoine Jijini Mbeya.

"Pamoja na Ujumbe mkuu Mwenge wa UHURU umeendelea kulisitiza mapambano dhidi ya Rushwa, Mapambano dhidi ya UKIMWI, Mapambano dhidi ya dawa zakulevyo na elimu juu ya Lishe" alisema Ismail Ussi

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania TACAIDS Dkt Samwel Sumba ameshukuru Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa mchango wake katika kusaidia

Bajeti ya mwaka wa fedha 2025–2026.

Sherehe za Madhimisho ya kuzima Mwenge wa Uhuru 2025 ziliambatana na maonesho ya wiki ya vijana kitaifa yaliyobeba kaulimbiu isemayo "Jitokeze kushiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kwa amani na Utulivu"

KAMATI YA UKAGUZI YA TACAIDS YASISITIZA UWAZI NA UWAJIBIKAJI



Kamati ya Ukaguzi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) imefanya kikao cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2025/2026, ambapo imeweza kujadili taarifa muhimu ikiwemo mapato na matumizi kwa robo ya kwanza, Manunuzi, Mpango wa mwaka wa ukaguzi wa ndani pamoja na taarifa za Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF).

kikao hicho kimeongozwa na Mwenyekiti wa kamati hiyo David Alal, Novemba 2025 mkoani Morogoro. Kamati hii ni moja ya mifumo inayohakikisha uwepo wa uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa afua za VVU na UKIMWI nchini.


TACAIDS YATOA MAFUNZO YA VVU NA UKIMWI KWA VIJANA WILAYA YA CHAMWINO

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania-TACAIDS kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino pamoja na wadau chini ya ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa (UNFPA) imetoa mafunzo kwa vijana wa kata ya Dabalo wilayani Chamwino kuhusu kujikinga na VVU na UKIMWI,

yanyapaa na Ubaguzi kwa Watu Wanaoiishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) pamoja na kuinga maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na elimu kuhusu Mwitikio wa UKIMWI nchini.

Mafunzo hayo yamefanyika Disemba 03, 2025 kwa lengo la kuwaongezea vijana uelewa katika masuala muhimu ya VVU na UKIMWI ikiwa ni pamoja na kuhamasisha vijana kuzifikia huduma za UKIMWI kama vile upimaji, huduma za Kinga, Matibabu na Matunzo ili kufikia malengo ya kutokomeza UKIMWI kama tishio la afya ya jamii ifikapo mwaka 2030.





TACAIDS YARATIBU UTOAJI WA MAFUNZO YA VVU NA UKIMWI DODOMA

Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa kushirikiana na wadau wa UKIMWI chini ya ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa (UNFPA) wametoa elimu kwa wananchi wa kata ya Viwandani jijini Dodoma kuhusu kujikinga na maambukizi ya VVU, matumizi sahihi ya Kondom, kupinga ubaguzi na un-

UKIMWI (WAVIU) na namna yakuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa Mtoto.

Utoaji huo wa elimu umeambatana na zoezi la upimaji wa VVU kwa hiari ambapo Jumla ya watu 16 wameweza kupima ikiwemo wanawake 5 na wanaume 11 na jumla wa watu 53 wamepatiwa vipimo vya jipime (Self-test kit).

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo Mratibu anaesimamia Afua za UKIMWI katika sekta za umma kutoka TACAIDS Dkt. Hafidh Ameir alisisitiza kuwa vijana ni kundi muhimu katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, hivyo ni lazima waongezewe maarifa ya kujikinga na VVU, kuhamasishwa ili waweze zo.

Aidha, ameeleza kuwa mafunzo haya ni sehemu ya jitihada za kitaifa za kufikia lengo la kudhibiti maambukizi mapya ya VVU ifikapo mwaka 2030.

Kwa upande wao, washiriki wa mafunzo wameelezea kufurahishwa na elimu waliyoipata na kuahidi kuwa mabalozi wazuri katika kupinga unyanyapaa, Kuhamasisha wenzao kujitokeza kupima na kutumia njia salama za kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU.



TACAIDS YAKUTANA NA WADAU WA AFUA ZA KONDOM TANZANIA BARA

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na wadau wanaotekeleza afua za Kondom wamefanya Mkutano wa Mwaka kwa lengo la kutathimini utekelezaji wa afua za kondom nchini.

Mkutano huwo umefanyika Disemba 5, 2025 jijini Dodoma, ambapo umejumuisha wadau mbalimbali wakiwemo wawakilishi wa usafiri wa bodaboda, wahudumu wa nyumba za wageni na kumbi za starehe kwa lengo la kuunganisha nguvu ya jamii katika kutoa elimu ya matumizi sahihi ya kondom na kuhakikisha inasambazwa kwa jamii.

Akizungumza wakati akifungua mkutano huwo Dkt. Thomas Rutachunzibwa, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, alisisitiza umuhimu wa wadau kuhakikisha elimu ya matumizi ya kondom inatolewa kwa jamii na kuhakikisha upatikanaji wake.

“Ni lazima tuwe na programu nyingi za uhamasishaji na uelimishaji ili kuhakikisha matumizi sahihi ya kondom yanaeleweka na kuenea nchini,” alisema Dkt. Rutachunzibwa.

Kwa upande wake, Dkt. Mariam Ngaje kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la idadi ya watu, Afya ya Uzazi na Haki za Kijinsia (UNFPA), ambaye alizungumza kwa niaba ya wadau, amesema kuna haja ya kuongeza mshikamano katika kuchochea kampeni za kuhamasisha matumizi sahihi na ende-

“Ipo haja ya kushirikiana zaidi ili jamii ipate kuelewa umuhimu wa kondom,” alisema Dkt. Ngaje.

Mkutano huu ulilenga kuongeza nguvu katika kuelimisha na kuhamasisha jamii hususani vijana kuhusu matumizi sahihi ya kondom, ili kupunguza maambukizi mapya ya VVU na kulinda afya ya uzazi nchini.




BODI YA ATF YAJIPANGA KUFIKIA MALENGO 2030

Bodi ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF) imefanya kikao cha utekelezaji kwa lengo la kuimarisha mikakati ya mfuko katika kuchangia juhudi za kitaifa kufikia malengo ya kutokomeza UKIMWI ifikapo mwaka 2030. Kikao hicho kimeongozwa na Mwenyekiti wa Bodi, Sabasaba

Katika kikao hicho, wajumbe wamejadili kwa kina namna ya kuongeza upatikanaji wa rasilimali za kutekeleza afua za VVU na UKIMWI pamoja na kuhamasisha sekta binafsi kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya maambukizi mapya na kuboresha huduma kwa watu wanaoishi na VVU.

Akizungumza kwa niaba ya Menejimenti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Kaimu Mkurugenzi Mtendaji, Dkt. Samwel Sumba, ameshukuru bodi ya ATF kwa kuendelea kushirikiana na Tume katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, ameomba bodi kuendeleza ushirikiano huo ili kuhakikisha Tanzania inafikia malengo ya kitaifa ya kudhibiti UKIMWI ifikapo 2030.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya ATF, Sabasaba Moshingi, amesema dhamira ya bodi ni kuendelea kuboresha mifumo ya upatikanaji wa rasilimali na kuimarisha ushirikiano na wadau wote, hususani sekta binafsi, ili kuongeza ufanisi wa mfuko huo katika kutekeleza majukumu yake. Kikao hicho ni sehemu ya mwendelezo wa mikakati ya ATF katika kuhakikisha mfuko unatekeleza wajibu wake kwa ufanisi na kuchangia kikamilifu katika mapambano ya UKIMWI nchini.



@tacaidinfo



@tacaidinfo



@tacaidinfo



@tacaidinfo

**Tume ya Kudhibiti
UKIMWI Tanzania**

S.L.P 2904

Nanenane, Nzuguni

DODOMA

Barua pepe:

info@tacaidinfo.go.tz

Tovuti:

www.tacaidinfo.go.tz